Ijumaa Tarehe 2/12/1427h=22/12/2006ad,P.o.box398 Pongwe-Tanga-Tanzania.makala namba 9.

# HII NDIYO DAAWA YETU

## JUU YA UFAHAMU WA SALAF SWALIH

**إِنَّ اللّهَ لاَ يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتَّى يُغَيِّرُواْ مَا بِأَنْفُسِهِمْ ....الرعد11**

"Hakika mwenyezi Mungu habadili  yaliyoko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo katika nafsi zao..".ar raad(13) aya 11.

**Muandishi;**

**Al akh Abul Fadh'li Qassim Mafuta Qassim.**

بسم الله الرحمن الرحيم

Ewe mola wetu ni zako wewe sifa njema zote,na shukrani zote, ni zako wewe sifa njema vile zinavyo lingana na utukufu wako,na ukubwa wako,ni zako wewe sifa njema mpaka uridhike,na pale unaporidhika, na baada ya kuridhika.

Na sala na salamu zimfikie kipenzi chetu,Mtume wetu Muhammad, na jamaa zake,na maswahaba zake wote,na walioiandama njia yao kwa wema mpaka siku ya malipo.

Katika mambo ambayo tunakubaliana waislamu wote wa zama hizi, ni kwamba waislamu wa zama hizi wanaishi katika hali ya unyonge usio na mfano ukilinganisha na hali ya makafiri.

Leo hii kila kona ya dunia unapofika waislamu wanalalama juu ya dhul'ma,na uonevu wanao upata kutoka kwa wasio kuwa waislamu, na kwabahati mbaya hakuna wakuvisikiliza vilio vya waislamu,bali kila uchao zinaundwa sheria na mbinu mbalimbali za kitaifa na kimataifa za kuwakandamiza waislamu,kuanzia zile za kisiasa hadi zile za mtutu wa bunduki.

Lakini pale unapo amua kuirudia historia sahihi ya waislamu waliotangulia utaikuta hali ni tofauti kabisa na waislamu wa sasa,na hapo ndipo utakapoanza kujiuliza maswali tofauti,lakini kubwa na la msingi ni pale utakapo jiuliza;

kwanini wale walikuwa katika hali ile,na sisi tuko katika hali hii?

-Ni upendeleo waliopewa na Allah? au ni ahadi walizo zitekeleza Wakastahiki kulipwa neema hiyo?

Pamoja nahayo bado kuna baadhi ya waislamu katika zama hizi hawaisi chochote juu ya madhila yote yanayo wasibu waislamu! na wanaona kwamba mambo ni shwari,lakini wengi wao niwale wasiyo na ghera na dini yao.

Na kuna wale walio ling'amua hilo,lakini hawakuweza kugundua siri,na kiini cha yote haya yanayo waumiza waislamu,na sababu kuu iliyowazuia kung'amua hilo ni ujinga wa kutoifahamu dini yao.

Na kuna wale wanaojifanya kuwa wameigundua siri ya matatizo,na wakaamua kuitafutia ufumbuzi wa haraka,utawaona wakipita kwa watu huku wakitweta tena kwa hamaki kubwa,na sauti zilizo jaa hamasa wakisema;

sababu za unyonge wetu,ni sisi waislamu;

-kukosa mshikamano!!
Waislamu hatuna umoja!!
Wengine husema;

Sababu ya unyonge wetu ni;
-kukosa dola,na uongozi!!! Waislamu hatuna dola yetu!!kwahiyo lazima tusimamishe dola ya kiislamu.

Wengine nao husema;

Sababu ya unyonge wetu ni;
-kukosa elimu,na teknolojia kama waliyo nayo makafiri!!

Wengine nao husema;
Sababu ya unyonge wetu ni;
-uchache wa mali kama walizo nazo makafiri!!!

Na mengine mengi yanayo tajwa kama ndiyo matatizo ya msingi,na watu wakenda mbiyo kuyatafutia ufumbuzi!!

## VYANZO VYA MADHILA KWA MTAZAMO WA SHERIA

Lakini sisi tunapo yatupia jicho maandiko ya kisheria tunakuta kwamba mitazamo iliyo tangulia bado haija gusa kwenye tatizo,bali imepapasa juu juu tu,hivyo basi hata ufumbuzi wake pia hautokuwa sahihi,mfano kwa wale wenye mtazamo wa kwamba sababu ya udhalili ni kukosekana mshikamano,utawaona wakisema;

Waislamu tuwacheni far'ka !!! tuweni kitu kimoja!!!
Na huku wakizifumbia macho sababu zinazo leta tofauti hizo na vyanzo vyake,mfano;

Mingoni mwa vyanzo vya far'ka ni uzushi (bid'a) katika dini,kama alivyoeleza Bwana Mtume s.a.w.lakini wenye kupigania umoja wa waislamu hawalioni jambo hili kuwa ni moja miongoni mwa vyanzo vya farka,na ndiyo maana hawakemei uzushi (bid'a) katika dini,bali mara

nyingine huunga mkono uzushi (bid'a) na huwa wakali katika kuwakemea wale wenye kupinga uzushi,na kuwaona wao kuwa ndiyo wanao sababisha far'ka!! Subhaanallah kweli tutafaulu sisi?!!

Bwana Mtume s.a.w. anasema;

فإنه من يعش منكم بعدي فسيرى اختلافا كثيرا
فعليكم بسنتي وسنة الخلفاء المهديين الراشدين تمسكوا بها وعضوا عليها بالنواجذ
وإياكم ومحدثات الأمور فإن كل محدثة بدعة وكل بدعة ضلالة

"Atakaye ishi miongoni mwenu atakuja kuziona tofauti nyingi mno
Basi (wakati huo) shikamaneni na Sunna zangu,na Sunna za Makhalifa waongofu wenye kuongoza,shikamaneni nazo,na mzing'ate kwa meno ya mwisho(zishikeni barabara wala msiziwache)
Na tahadhrini na Uzushi(BID'A) katika mambo(ya dini) ,kwasababu kila uzushi ni bid'a,na kila bid'a ni upotevu".

Tazama Sunan Abi Daud,juz2 uk610,hadithi namba4607.

Na ama wale wenye mtazamo wa kwamba sababu ya udhalili wetu ni kukosa dola/ukhalifa utawasikia wakisema;
Waislamu lazima tuwe na dola yetu,na uongozi wetu,tusikubali kumtii twaghuti…!!

Huku wakiwa macho yao yote wameyaelekeza ikulu,na huku ute uki wachuruzika kwa uchu wa madaraka,na zikawa fikra zao hazipituki kabla ya kuja mkoloni!

Bila shaka hawa na wengineo hawawezi kufaulu.
Ama kiislamu, hakuna mabadliko yoyote yanayo weza kuwafika watu,ya kheri wala ya shari isipokuwa kwa mabadiliko ya nyoyo zilizomo vifuani mwao.

Watu wanapokuwa katika neema,neema hiyo haiwezi kuondoka ila kwa watu(waislamu) kuikufuru neema hiyo,amesema Allah s.w.t;

ذَلِكَ بِأَنَّ اللّهَ لَمْ يَكُ مُغَيِّراً نِّعْمَةً أَنْعَمَهَا عَلَى قَوْمٍ حَتَّى يُغَيِّرُواْ مَا بِأَنفُسِهِمْ ....} الأنفال53{

"Hayo (yakuwafika balaa hizi) ni kwa sababu mwenyezi Mungu habadilishi kabisa neema alizowaneemesha watu,hata wabadilishe wao yaliyomo nyoyoni mwao…." Al anfal(8) aya53.
na bila shaka kila aliye na insafu atakubaliana na mimi kwamba waislamu wenzetu waliotangulia walikuwa katika neema ya izza,ushindi,na kuitawala dunia,swali je neema hiyo tuko nayo?

Jawabu,la
Swali, kwanini?

Jawabu,ni mabadiliko ya nafsi zetu,badala ya tawheed tumeweka shir'ki,badala ya sunna tumeweka bid'a,badala ya kushukuru neema kwa amali njema tumeweka kuf'ru,na kibri.

Na ama watu wanapo kuwa katika balaa,dhiki,tabu,na madhila yoyote yale,hawawezi kupata faraja ila kwa kumbadilikia mwenyezi mungu,amesema Allah s.w.t;

**إِنَّ اللّهَ لاَ يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتَّى يُغَيِّرُواْ مَا بِأَنْفُسِهِمْ  الرعد11**

"Hakika mwenyezi Mungu habadili  yaliyoko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo katika nafsi zao..".ar raad(13) aya 11.

Ama katika sunna za mtume s.a.w. kuna hadithi nyingi zilizo na maana kama hii,miongoni mwa hizo ni ile isemayo;

**قال صلى الله عليه و سلم : يا معشر المهاجرين خمس إن ابتليتم بهن و نزل فيكم أعوذ بالله أن تدركوهن:**
**1- لم تظهر الفاحشة في قوم قط حتى يعملوا بها إلا ظهر فيهم الطاعون و الأوجاع التي لم يكن مضت في أسلافهم.**
**2-و لم ينقصوا المكيال و الميزان إلا أخذوا بالسنين و شدة المؤنة و جور السلطان عليهم.**
**3-و لم يمنعوا الزكاة إلا منعوا القطر من السماء و لولا البهائم لم يمطروا.**
**4-و لم ينقضوا عهد الله و عهد رسوله إلا سلط عليهم عدوهم من غيرهم و أخذوا بعض ما كان فى أيديهم.**
**5-و ما لم يحكم أئمتهم بكتاب الله إلا ألقى الله بأسهم بينهم.**

Amesema mtume s.a.w;
"Enyi muhajirina! Iwapo mtapewa mtihani katika mambo matano,na yakakushukieni-nina muomba Mwenyezi Mungu- yasikufikeni;
1-hautodhihiri uchafu katika jamii yoyote,mpaka ukatangaa isipokuwa yataenea maradhi ya mlipuko,na maradhi mengine ambayo hayakuweko kwa watu walio tangulia.

2-watu hawato punguza vipimo,isipokuwa wataadhibiwa, kwa njaa kali,gharama ya vitu,na utawala katili juu yao.
3- hawato zuia zaka za mali zao isipokuwa watanyimwa mvua (za baraka) kutoka mbinguni,na lau si wanyama wasingepewa mvua.

4-hawato zivunja ahadi za Mungu,na Mtume wake,isipokuwa Allah atawasaliti na maadui zao,na(maadui) watavichukua baadhi ya (vitu) vilivyomo mikononi mwao(k.v.utaalamu,utajiri,nidhamu ya mambo mbalimbali n.k).

5-na kama viongozi (watawala) hawato wahukumu watu na kitabu cha Allah(Qur'an) isipokuwa vita vyao vitakuwa baina yao (wenyewe kwa wenyewe).

Bila shaka muislamu aliye na ghera ya uislamu akizitafakari kwa undani nususi hizi za kisheria ataanza kubainikiwa na vyanzo vya masaibu yanayo wafika waislamu hii leo,na atafahamu kwamba;

-maradhi haya ya hatari vyanzo vyake ni kuenea ufuska.

-njaa,gharama za maisha,utawala dhalimu,ni natija ya utapeli,na kupunguza vipimo.

-mvua za maangamivu,au kutokuwepo kabisa ni kwasababu ya ubakhili unaopelekea kuzuia zaka.

-usaliti wa maadui dhidi ya waislamu,mpaka kufikia kuporwa ardhi zao,mali zao,ustaarabu wao nk,ni natija ya kuvunja ahadi ya Allah na mtume wake s.a.w.ahadi ambayo ni kushikamana na dini ya Allah s.w.t.(uislamu) na kuitetea.

-ugomvi,farka,kukosekana mshikamano wa kweli,sababu ni kuwa mbali na kitabu cha Allah s..w.t.

## JE UONGOZI (KHILAFA)NDIYO LENGO AU NI NJIA YA KUFIKIA LENGO?

Kwabahati mbaya kabisa ni kwamba waislamu wengi wanashindwa kutofautisha kati ya vitu viwili hivi;

1-wasila (njia) na

2-ghaya (lengo)
Mpaka mara nyingine ikafikia njia kufanywa kuwa ndiyo lengo,na lile lengo likawa ni njia tu ya kutufikisha.

Na hivyo ndivyo lilivyo eleweka suala zima la khilafa (uongozi) katika mtazamo wa baadhi ya waislamu wa zama hizi,utawaona wengi wao wakihangaika na kwenda mbio huku jasho likiwakatika, ukiuliza kulikoni?

Utaambiwa kwamba tuko katika harakati za kusimamisha dola !

Swali,je waislamu waliotangulia walikuwa na dola au la?

Bila shaka jawabu litakuwa ndiyo walikuwa na dola,
na kama ni hivyo,je ni zipi sababu zilizofanya kuanguka kwa dola hiyo? Na je tumeshafanya juhudi ya kuziondoa sababu hizo? Kama bado hatuja ziondoa sababu hizo,hatuoni kwamba tunatafuta jambo lililo muhali? Kuwa na khilafa(Dola) ni moja kati ya njia za kutusahlilishia,kufikia lengo kuu la kuumbwa kwa viumbe,nalo ni kumuabudu Allah pekeyake bila ya kumshirikisha na kitu chochote,amesema Allah s.w.t;

**{وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ }الذاريات56**

"Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu".ad dhaariyat(51)aya ya 56.
Na kwenye lengo hilo ndiyo ulikuwa ulinganizi wa Mitume wote,ni mamoja walikuwa na Dola au la,amesema Allah;

**{وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولاً أَنِ اعْبُدُواْ اللّهَ وَاجْتَنِبُواْ الطَّاغُوتَ ....}النحل36**
"Na bila shaka tulimpeleka Mtume katika kila uma ya kwamba Muabuduni Mwenyezi Mungu na mwepukeni (Iblisi) muovu…."
An nah'l(16) aya ya 36.

JE NI NANI ALIYE NA JUKUMU LA KUSIMAMISHA KHILAFA (DOLA)?

Swali hili lina jibiwa na aya ya 55,ya surat nuur(24),isemayo;

**وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُم فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَى لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْناً يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئاً وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُوْلَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ }النور 55**

"Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri,kuwa atawafanya makhalifa katika ar'dhi kama alivyowafanya makhalifa wale waliokuwako kabla yao,na kwa yakini atawasimamishia dini yao aliyowapendelea,na atawabadilishia amani

baada ya hofu yao,wawe wananiabudu,hawanishirikishi na chochote.Na watakao kufuru baada ya hayo,basi hao ndiyo wavunjao amri zetu".

Mpaka hapo ndugu muislamu utakuwa umegundua kwamba,suala la kusimamisha ukhalifa si jukumu letu sisi waislamu,
bali kusimama khilafa ni ahadi ya Mungu,ahadi ambayo Mungu atawatimizia watu wenye sifa maaalumu,
na uzuri wa mambo ni kwamba,waislamu wote tunakubaliana kwamba Allah s.w.t. katu haendi kinyume na ahadi anazo zitoa kwa waja wake.

Hapo katika aya iliyo tangulia tumeona kuwa;
Allah amewaahidi,
-Wale walio amini,
-na kutenda vitendo vizuri,
Swali muhimu la kujiuliza ni;

Kina nani hao walioamini? Wameamini nini? Na yeye kwasasa anaamini nini?na je hiyo imani yake ni kama yao? ni vipi hivyo vitendo vizuri? Ni vile alivyo kuja navyo Mtume s.a.w.? au ni vile alivyo virithi kutoka kwa wazee,na wahenga wake?

Maana Allah anasema;

**{فَإِنْ آمَنُواْ بِمِثْلِ مَا آمَنتُم بِهِ فَقَدِ اهْتَدَواْ وَّإِن تَوَلَّوْاْ فَإِنَّمَا هُمْ فِي شِقَاقٍ فَسَيَكْفِيكَهُمُ اللّهُ وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ } البقرة137**

"Basi wakiamini kama mnavyoamini (nyinyi) itakuwa kweli wameongoka.Na wakikengeuka basi wao wamo katika upinzanitu.Basi Mwenyezi Mungu atakukinga na shari yao,na yeye ndiye asikiaye ajuaye". Albaqarah(2) aya 137.

Na amesema Mtume s.a.w;

**من عمل عملاً ليس عليه أمرنا فهو رد**

Mwenye kutenda amali ambayo haimo(haikufundishwa) katika dini yetu,basi amali hiyo(itarudishwa) haito kubaliwa.

Na je Allah amewaahidi nini hao walioamini na kutenda vitendo vizuri?

-amewaahidi kuwa atawafanya makhalifa (watawala) katika ar'dhi,kama alivyo wafanya makhalifa walio kabla yao,na bila shaka hili kwasasa halipo.

-atawasimamishia dini yao aliyo wapendelea,bila shaka kwasasa dini imetwezwa,na kutupiliwa mbali.

-atawabadilishia amani baada ya hofu,bila shaka hivi sasa waislamu wenye kushikamana na dini yao barabara wamejawa na hofu juu udhalimu wa makafiri na vibaraka wao.

Lengo ya haya yote ni nini?

Wawe wanamuabudu Allah s.w.t.bila ya kumshirikisha na kitu chochote.
Na hili ndiyo lengo la kuumbwa mwanaadamu,amesema Allah;

**{وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ }الذاريات56**

"Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu".ad dhaariyat(51)aya ya 56.

Kwa muktadha wa aya hizi ni kwamba wajibu wa waislamu kwa wakati wasasa ni;

kutimiza mashar'ti ili Allah atekeleze ahadi yake,

na mfano wa watu wenye kuhalifu utaratibu huu,kwa kutaka kupata khilafa(dola) kupitia mali au nguvu za kijeshi,au kuleta mshikamano feki wa viwiliwili,na wakawa wanaiona njia hii ya Allah na Mtume wake kuwa ni ndefu,na ni ngumu,kwahiyo wakaamua kufuata njia ya mkato, mfano wa watu hao ni sawa na mtoto aliye ambiwa na mzazi wake;
Mwanangu ukisoma elimu ya msingi ukafaulu,kisha secondary,na chuo ukapata degree nitakujengea nyumba nzuri,na kukutafutia ajira yenye mshahara mnono kabisa!
Mara ukamuona mtoto huyo anaminyana kukusanya mchanga,na kuanza kufyatua tofali!
yuko mbioni hali,wala hanywi kwa raha! halafu ukimuuliza kwanini unataabika namna hiyo? ana kwambia kwamba;
Baba ameniahidi ni kifaulu atanijengea nyumba!!

Je mtoto huyo atakuwa ameyaelewa maneno ya baba yake?

Na je atakuwa amechukua hatua za msingi ili kutimiziwa ahadi aliyo pewa?

Bila shaka jawabu litakuwa hapana.

Mfano wa kijana huyo ni kama hawa wanao kwenda mbio wakitafuta hiyo iitwayo dola ya kiislamu,bila ya kuyazingatia yaliyo sababisha kuanguka kwa dola hiyo.

Bila ya kujilazimisha kutimiza masharti  waliyo wekewa,
Bila ya kutaka kujua malengo ya utawala huo,
Bila ya kuchukua hatua ya kujibadilisha nafsi zao,
Na hapo nyuma amesema msemaji mmoja;

Simamisheni dola ya kiislamu katika vifua vyenu,na Allah ataisimamisha katika nchi zenu!!

Bila shaka wale wanao kwenda kinyume na utaratibu wa Allah na Mtume wake ni watu waliozugwa akili zao na  wanatafuta jambo la   muhali, hawajui kwamba nchi ni za Mwenyezi Mungu anammilikisha amtakaye katika waja wake?!

## USIA WA NABII MUSA A.S. KWA WANA WA ISRAEL

Basi hapa ninawakumbusha Usia wa Musa kwa kaumu yake alipowaambia;

**قَالَ مُوسَى لِقَوْمِهِ اسْتَعِينُوا بِاللّهِ وَاصْبِرُواْ إِنَّ الأَرْضَ لِلّهِ يُورِثُهَا مَن يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ وَالْعَاقِبَةُ لِلْمُتَّقِينَ**
**قَالُواْ أُوذِينَا مِن قَبْلِ أَن تَأْتِينَا وَمِن بَعْدِ مَا جِئْتَنَا قَالَ عَسَى رَبُّكُمْ أَن يُهْلِكَ عَدُوَّكُمْ وَيَسْتَخْلِفَكُمْ فِي الأَرْضِ فَيَنظُرَ كَيْفَ تَعْمَلُونَ }الأعراف{الأعراف128-129.**

"Musa akawaambia kaumu yake "Ombeni msaada kwa Mwenyezi Mungu na Subirini.Ardhi ni ya Mwenyezi Mungu atamrithisha amtakaye katika waja wake,na mwisho(mwema ) ni kwa wamchao.
Wakasema "Tumeudhiwa kabla hujatufikia na (pia sasa)baada ya wewe kutujia"(Musa)akasema: "Asaa Mola wenu atamwangamiza adui yenu na kukufanyeni watawala katika nchi (hizi) na aonejinsi mtakavyofanya."
Al aaraf(7) aya 128-129. "

## WASIFU WA KIONGOZI WA DOLA YA KIISLAMU (KHALIFA).

Miongoni mwa mambo muhimu ambayo yanapaswa kuangaliwa kwa undani zaidi ni kuhusiana na suala zima la wasifu wa kiongozi wa kiislamu na kujua pia mahali anapo tengenezwa,

Je kiongozi (khalifa) anasifa zipi?
Na anatengenezwa wapi?
China,India,Amerika,au Ulaya?

Na ukisha ujua wasifu wa kiongozi(khalifa) wa kiislamu ndiyo utajua kwamba anatengenezwa wapi,na pia utajua ni wakati gani utatumika kumuandaa kiongozi huyo/viongozi hao.

Je ni kabla ya kupata dola au baada?
Pia utafahamu umuhimu wa kuwaandaa raia ambao wanatarajiwa kuwa chini ya kivuli cha uislamu,je haya yote ni baada ya dola au ni kabla?
Yote ni kwa kuhofia yale aliyo yasema Allah s.w.t;

**{فَهَلْ عَسَيْتُمْ إِن تَوَلَّيْتُمْ أَن تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ وَتُقَطِّعُوا أَرْحَامَكُمْ }محمد22**

"Ndiyo yanayotarajiwa kwenu kufisidi  katika ardhi na kuwakata jamaa zenu wakati mkipata ukubwa".
surat Muhammad(47)aya22.

Hizi ni baadhi ya sifa ambazo anatakikana awe nazo kiongozi wa Dola ya kiislamu;

1-Awe muislamu,mcha Mungu
-kwa tafsiri yakiislamu,na si kwa tafsiri ya wanasiasa-
2-Awe na elimu ya kumtambua Allah(elimu ya Qur'an na Sunna).
3-Awe na yakini juu ya imani ya kiislamu.
4-Awe mwanamme,asiwe mwanamke.
5-Awe na akili timamu,asiwe mwenda wazimu.
6-Awe na afya njema,asiwe na maradhi yatakayo muathiri katika shughuli za uendashi wa dola.

Na nyinginezo ambazo wamezitaja wanawachuoni katika vitabu vya fiqhi.

Ukiyaangalia kwa makini mashar'ti tuliyo yapigia mstari utagundua kwamba maandalizi ya kumuandaa kiongozi si ya muda mfupi,
Na hasa ukizingatia kwamba kiongozi  hatoki mbinguni,wala katika jamii ya malaika,bali anatokana katika jamii yetu, katika familia zetu,katika miji yetu,na nchi zetu,hivyo tuna kazi kubwa ya kuyasafisha mazingira yetu kwa lengo la kumpata kiongozi bora,na si bora kiongozi.

Basi kwanini yasiimarishwe mazingira ya kumtoa kiongozi huyu,na kuyaboreshwa,au kuasisiwa kikamilifu kama hayapo,au maandalizi ni mpaka baada ya kupata khilafa? Je hatuoni kwamba hicho ni kinyume cha mambo?

Mantiki ya maneno haya ni kwamba,kwanini tusiyaendee mambo kupitia milango yake,na kufuata taratibu zake?
Kwa ufupi; tuachane na mambo yasiyo tuhusu,na tulishughulikie lile linalo tuhusu.

Na jambo kubwa linalo tuhusu sisi ni kusimamisha dola ya kiislamu katika vifua vyetu,na katika nyumba kwanza,ili Allah s.w.t. atutekelezee ahadi yake ya kutusimamishia dola katika nchi zetu.
Na hili haliwezi kuwa mpaka;

wawe wake zetu,mama zetu,dada zetu,katika kuzitekeleza amri za Mungu kama vile walivyokuwa wanawake wa Ansaar wa Madina wakati ilipoteremka amri ya Allah ya kuvaa hijabu,habari zilipo fika katika nyumba zao hapohapo amri ikaanza kutekelezwa, tena hata Bwana Mtume s.a.w. alikuwa hajaondoka katika majlisi yake ile, mara wakaonekana wanawake wakipita njiani huku wamevaa hijabu bila ya kusubiri mpaka kesho!!

Mpaka tuwe kama maswahaba wa Bwana Mtume s.a.w. katika kuacha yale yaliyo katazwa,kama vile siku ile iliposhuka aya ya kukataza kunywa ulevi milele,palepale wakaelekea katika nyumba zao na kuanza kuimwaga mitungi ya pombe,na hali yakuwa kuna baadhi yao wameitia mitaji yao na rasili mali zao katika biashara ya pombe,lakini hawa kungojea mpaka wauze ili mtaji urudi,bali walimuitikia Allah na Mtume wake bila ya simile,
ALLAHU AKBAR!!!
Mpaka tuwe kama swahaba Mai'z bin Malik pindi alipoteleza na kufanya dhambi ya zinaa alikuwa radhi kusimamishiwa amri ya Allah juu yake nayo ni kupigwa mawe mpaka kufa!! Tena aliljileta mwenyewe wala hakusubiri kuletewa karandinga limsombe kama mzigo,maana dola ikisimama ni hukumu ya Allah ndiyo itakayo tekelezwa bila ya upendeleo,wala dhulma.

Mpaka wawe watoto wetu katika kupenda kuinusuru dini ya Allah kama kina Ibin Umar ambao walikuwa wakililia kwenda vitani kuinusuru dini ya Allah na hali wakijua kwamba huko hakuna pipi,wala biscuit, hakuna gololi wala pool,hakuna video wala

game,bali huko hakuna zaidi ya panga na mikuki,nakutolewa roho,au kukatwa kiungo!!

Mwisho kabisa labda nimalizie na hadithi ya Bwana Mtume s.a.w. hadithi ambayo inatufafanulia hali halisi tuliyo nayo;

قال رسول الله صلى الله عليه وسلم :
يوشك الأمم أن تداعى عليكم كما تداعى الأكلة إلى قصعتها " فقال قائل ومن قلة نحن يومئذ ؟
قال " بل أنتم يومئذ كثير ولكنكم غثاء ( ما يحمله السيل من وسخ ) كغثاء السيل
ولينزعن الله من صدور عدوكم المهابة منكم
وليقذفن الله في قلوبكم الوهن "
فقال قائل يارسول الله وما الوهن ؟
قال " حب الدنيا وكراهية الموت " .
صحيح :قال الشيخ الألباني

"Mataifa yanakaribia kuitana kwa ajili yenu nyinyi (waislamu) kama wanavyoitana walaji kwenye sahani ya chakula!
Akauliza mtu mmoja;
je nikutokana na uchache wetu kwa kipindi hicho?!
Akasema (Mtume s.a.w.); hapana,nyinyi wakati huo mtakuwa ni wengi,lakini mtakuwa ni povu tu,kama povu linalo bebwa na maji ya mvua,
Na Allah ataondosha hofu katika nyoyo za maadui zenu(hawato waagopeni tena)
Na na ataingiza katika nyoyo zenu (maradhi ya) Wah'ni !
Akauliza muulizaji mmoja ni nini maana ya wah'ni Ewe Mtume wa Mungu?
Akasema Mtume s.a.w;
Wah'ni ni kupenda sana dunia,na kuyachukia mauti".

Tazama sunan Abi Daud,juz 2,uk514,hadithi namba 4297,chapa ya darul fikri Beirut-Lebanon.

Kwa uwazi huu alioutoa Bwana Mtume s.a.w. si dhani kwamba hadithi hii itahitaji maelezo marefu.

Bila shaka  kwa kupenda kwetu dunia ndiyo tukafikia kutoa nyudhuru za kuacha ibada kama swala kwa kisingizio cha kubanwa na kazi,au shughuli nyingi au maradhi n,k.!!

Kwa kupenda kwetu dunia ndiyo tukafikia kuwa tayari kuwasomesha watoto wetu elimu ya kutafuta tonge kwa gharama zozote zile,popote pale,
kwa wakati wowote ule,tena kwa kisingizio kwamba eti nasisi waislamu tunahitaji mafundi bomba,umeme, madaktari n.k*
na tukawa ni wazito katika kuwaelimisha dini yao,tena hata yale mambo ya wajibu katika maisha yao ya kila siku, k.v kumtambua mola wao,kukijua kitabu cha mola wao,anasema nini,na anataka nini?kujua mafundisho ya Mtume wao s.a.w. na Utaratibu mzima wa kutekeleza ibada!

Bila shaka kwa hali hii tunastahiki kuitwa GHUTHAUN (povu linalo bebwa na maji ya mvua).

Bila shaka ndugu yangu muislamu bado tunayo kazi kubwa sana ya kuiondoa hali hii kwanza kabla ya jambo lolote.

Hebu ndugu yangu katika imani niambie ukweli,je sisi hatuko hivyo? Na mpaka sisi kufikishwa hapa na maadui madhalimu,ninani wa kulaumiwa kwanza?

---

* siyo kusudio langu kwamba kusoma elimu ya kuijua dunia ni haramu,la hasha!! Bali nina kusudia kuleta uwiano baina ya elimu ya lazima kwa kila muislamu,namna tunavyoipuuza,na elimu ambayo ni lazima kwa baadhi ya waislamu tu,na namna tulivyo kuwa mabingwa wa kutia hila katika mambo ya dini,tunatafuta dunia yetu kwa jina la kuitumikia dini? wangapi wanafungua shule kwa jina la dini? Wangapi wanaosoma kwa jina la kutaka kuitumikia dini,tena mpaka kufikia kutumika mali za waislamu matokeo yake kumbe ni mambo binasfi?! Mara ngapi waislamu wametapeliwa katika hili?
Je ni maadui? Viongozi wetu?masheikh zetu? waalimu wetu wa dini? Jamii yetu? Wazazi/walezi wetu?

Mimi ninasema kwamba;

Kila mmoja wetu aanze kuilaumu nafsi yake,na aanze kuchukua hatua za kuiondoa hali hii,kabla ya kuanza kutupa lawama kwa wenzake,aitazame kwanza nafsi yake,mke wake/mume wake,watoto wake wakike na wakiume,namna alivyo faulu au aluvyo feli katika kuujenga uislamu kimatendo katika nafsi yake,na jamii iliyo mzunguka,kwasababu familia(baba,mama,na watoto) ndiyo wanaounda nyumba ya kiislamu,

nyumba ndizo zinazo unda mtaa,mitaa ndiyo inayo unda mji,na miji inaunda nchi.

Na katika kuharibu ni vivyo hivyo.
Kwamfano kila mkazi katika  nyumba anatekeleza wajibu wake wa usafi wa mazingira yake,bila shaka nyumba zitakuwa safi,na mtaa utapendezana,na mji bila shaka utakuwa msafi,lakini pale unapokuwa mvivu ukasubiri watu wa city/manispaa waje wakusafishie choo chako ndipo mtaa utakapo anza kutoa harufu,na hapo lawama zisizo za msingi zitakapo anza.

## HATIMA

## UFUMBUZI WA MATATIZO YETU

Tutaweza kufikia ufumbuzi wa matatizo yetu kwa njia hizi zifuatazo;

1-Kufahamu kiini cha matatizo yetu,(nilipi tatizo halisi)
Tukifanikiwa jambo hili,basi bila shaka tutaweza kupata yafuatayo;
a)Ufumbuzi muafaka.
b)Kuondokewa na usumbufu wa kubuni viini feki,jambo ambalo lina tusababishia kupata ufumbuzi feki,mfano wahilo ni;
-Kama wale wanao waambia watu kila siku;
WAISLAMU TUWE KITU KIMOJA TUWACHENI FAR'KA!!

Huku wakivifumbia macho viini vya far'ka!

Ukweli ni kwamba far'ka imekatazwa katika safu za waislamu,
lakini pia lazima tufahamu kwamba farka ni lazima itokee, na kuna sababu za msingi zinazo sababisha kutokea farka.

Na pia ifahamike kwamba kunataratibu za kisheria za kuondoa farka, na miongoni mwa taratibu hizo ni kujihukumu kwa Qur'an,na Sunna sahihi za Mtume s.a.w. kama walivyofahamu wema aliotangulia pale inapotokea hali ya kukhitalifiana.

Amesema Allah;

فَإِن تَنَازَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللّهِ وَالرَّسُولِ إِن كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللّهِ وَالْيَوْمِ الآخِرِ ذَلِكَ خَيْرٌ
وَأَحْسَنُ تَأْوِيلاً

Na kama mkikhitilafiana juu ya jambo lolote basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume,ikiwa mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho,hiyo ndiyo kheri,na ina matokeo bora kabisa.
An nisaa (4) aya 59.

Ama kuwaambia watu wasitofautiane na hali tayari wameshatofautiana, au kudhani kwamba kumkataza aliye kinyume na Sunna za Mtume s.a.w. ni kukuza mzozo, hiyo ni namna za hila ya kutaka kuificha haki isijulikane,ni kweli kuna tofauti ambazo waislamu wanatakikana wazijue kuwa hizo ni za kawaida ndani ya safu,ni tofauti gani hizo?

Wanawachuoni wamezielezea katika vitabu vya fiq'hi.

Ama tofauti katika mambo ya kiitikadi kama vile;

Tofauti juu ya kumjua Allah majina yake na sifa zake .
Tofauti juu ya Mtume s.a.w. juu ya maswahaba,juu ya kuifahamu Qur'an na Sunna,n,k.tofauti hizo ni lazima ziondolewe,kwa kukemewa vikali aliye kwenye batili.,na watu wafahamu kwamba yuko kwenye batili,na aliye kwenye haki aungwe mkono na watu wafahamu kwamba yuko katika haki.

-Au kama wale wanaopita wakiwaambia watu;

WAISLAMU TUSIMAMISHE DOLA YETU,NA TUSIWAACHIE MAKAFIRI WATUTAWALE!!

Huku wakizifumbia macho sababu zote za kusimamisha dola,na wakawa wanadhani kwamba dola ya kiislamu itasimama kupitia masanduku ya uchaguzi,au kupitia badhi ya vyama vya siasa,na wakaweka matumaini yao huko bila shaka watu hao hawatofanikiwa katika juhudi zao hizo !!

2- Kuzifuata njia sahihi zilizowekwa na sheria katika kupambana na matatizo yote yanayo ukabili uma huu mtukufu,tena hata kama njia hiyo itaonekana kuwa ni ndefu na ni ngumu,lakini tufahamu kwamba kwenye njia hiyo ndiko iliko nusra.

3-Kupambana katika kuleta mabadiliko katika nafsi zetu kwanza kabla ya kutoa lawama kwa maadui,viongozi,n,k.

Na mabadiliko haya yatapatikana kwa;

-Kushikamana na kitabu cha Allah,na Sunna za Mtume s.a.w. kama walivyofahamu wema walio tangulia (SALAF SWALIH).

-Kupandikiza Tawheed katika nyoyo zetu,na watoto wetu,na wote walio chini ya usimamizi wetu.

-Kuipiga vita shirki,na mila zote za kishirikina.

-Kupiga vita sampuli zote za uzushi katika dini,hata kama tunauona kuwa ni mzuri,kwasababu dini imeshakamilika,na yule aliyetufaradhishia ibada hakusahau kutuwekea mitindo,na taratibu zake.

-Kushikamana na maadili mema ya kiislamu,na kuzitupilia mbali mila,desturi,tamaduni,na maadili yote yaliyo kinyume na uislamu.

-Nyumba za ibada zichukue nafasi yake ya kutoa mafundisho sahihi ya dini badala ya kuwa ni vituo vya habari za kuwatisha waislamu na adui yao,kwa mfano utamkuta Hatibu yuko juu ya mimbari anasema;

Ndugu waislamu,katika habari za gazeti la jana makafiri wamekaa kutujadili sisi waislamu,na wamepanga kadha wakadhaa!!
Kwa hamasa kali kabisa,badala ya kufahamishwa wajibu wao ili wasifikwe na hali hii.

Na mwisho wa yote hayo utasikia sauti za baadhi maamuma-tena huwenda ikawa bado Hatibu yuko juu ya mimbari- zikisema;

**Laatullahi alayh !!**

Na huwenda hapo hapo ikaanza safari ya (maandamano) kwenda kushitaki kwa huyo huyo kafiri anaye tujadili.

Ukweli ni kwamba makafiri  kila uchao wanatujadili,jambo la msingi kwetu kulijua ni kwanini tumefikia /kufikishwa hapa? tumekosea wapi?lipi la kufanya ili hali hii iondoke?

Hebu misikiti yetu ielimishe hili kwanza,sisi ni umma wenye izza, umma uliojuu wenye kushinda,ama hizi hila za makafiri na nguvu zao ni ndogo mno mbele ya Allah s.w.t.kama utaukumbuka wasia wa Musa a.s. kwa wana wa Israel alipowaambia;

"Asaa Mola wenu akamwangamiza adui yenu na kukufanyeni watawala katika nchi (hizi)…

<u>MAKALA; HII NDIYO DAAWA YETU</u>

-Ni Makala zinazo walingania wislamu kurudi na kushikamana na kitabu cha Allah,na Sunna sahihi za Mtume s.a.w. juu ya ufahamu wa wema walio tangulia.

-Kuwalingania watu kuzibadilisha nafsi zao kwanza kimatendo,na kuzisafisha nyoyo,jamii na ushirikina,bid'a,ufuska,na kuitanguliza dunia mbele kuliko mapenzi ya dini.

-Malezi bora juu ya misingi ya Tawheed,kufuata mafundisho ya Mtume s.a.w. kwa vitendo.

-Kuhuisha maadili mema ya kiislamu,na kuzipiga vita tamaduni,na maadili yote maovu.

-Kuwajenga watu juu ya misingi ya kielimu,badala ya kuwatia hamasa zisizo na msingi wowote.

-Kuleta mshikamano wa kweli wa kiroho kwa kujifunga sote na mafundisho ya Qur'an,na Sunna juu ya ufahamu wa SALAF SWALIH.

-Kupiga vita mishikamano yote feki,mishikamano ya viwiliwili na hali nyoyo ziko tofauti,kama umoja wa mayahudi,
"Utawadhania wao wako pamoja;kumbe nyoyo zao ni mbalimbali.Hayo ni kwasababu wao ni watu wasio na akili". Al hashr (59) aya ya 14.

-Kuwahimiza waislamu kushikamana na haki,na kuwa na subra juu ya yote yanayo wasibu,kwa kushikamana na hayo bila shaka faraja iko karibu.

Huku tukiiweka mbele yetu kauli za Allah s.w.t:

**إِنَّ اللّهَ لاَ يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتَّى يُغَيِّرُواْ مَا بِأَنْفُسِهِمْ الرعد11**

"Hakika mwenyezi Mungu habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo katika nafsi zao..".ar raad(13) aya 11.

قَالَ مُوسَى لِقَوْمِهِ اسْتَعِينُوا بِاللّهِ وَاصْبِرُواْ إِنَّ الأَرْضَ لِلّهِ يُورِثُهَا مَن يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ وَالْعَاقِبَةُ لِلْمُتَّقِينَ
قَالُواْ أُوذِينَا مِن قَبْلِ أَن تَأْتِينَا وَمِن بَعْدِ مَا جِئْتَنَا قَالَ عَسَى رَبُّكُمْ أَن يُهْلِكَ عَدُوَّكُمْ وَيَسْتَخْلِفَكُمْ فِي الأَرْضِ فَيَنظُرَ كَيْفَ تَعْمَلُونَ }الأعراف128-129.

"Musa akawaambia kaumu yake "Ombeni msaada kwa Mwenyezi Mungu na Subirini.Ardhi ni ya Mwenyezi Mungu atamrithisha amtakaye katika waja wake,na mwisho(mwema ) ni kwa wamchao.
Wakasema "Tumeudhiwa kabla hujatufikia na (pia sasa)baada ya wewe kutujia"(Musa)akasema: "Asaa Mola wenu akamwangamiza adui yenu na kukufanyeni watawala katika nchi (hizi) na aone jinsi mtakavyofanya".

Al aaraf(7) aya 128-129.

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُم فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَى لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْناً يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئاً وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُوْلَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ }النور 55

"Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri,kuwa atawafanya makhalifa katika ar'dhi kama alivyowafanya makhalifa wale waliokuwako kabla yao,na kwa yakini atawasimamishia dini yao aliyowapendelea,na atawabadilishia amani baada ya hofu yao,wawe wananiabudu hawanishirikishi na chochote. Na watakao kufuru baada ya hayo,basi hao ndiyo mafasiki (wavunjao amri zetu)".

وصلى الله وسلم وبارك على نبينا محمد وعلى آله وصحبه أجمعين
والحمد لله أولاً وآخراً